# MKATABA WA MAUZIANO YA SHAMBA

Mkataba huu unafanyika leo hii tarehe……31…… Mwezi ……12……………2024

**KATI YA**

**NDG.BASHU YALUGALA SAHANI wa S.L.P 610 KIJIJI CHA KINYAMWE KATA YA MAGIRI UYUI- TABORA,** (ambaye katika mkataba huu anajulikana kama 'Muuzaji' *neno ambalo litajumuisha mwenyewe pamoja mwenza wake wa ndoa, warithi wao na yeyote atakae dai haki kwa niaba yake katika mkataba huu)* kwa upande mmoja.

**NA**

**MH. HUSSEIN MOHAMMED BASHE WA S.L.P 106, NZEGA – TABORA,** *(ambaye kati ya mkataba huu anajulikana kama "Mnunuzi "jina ambalo litajumuisha yeye pamoja na yeyote atakayedai haki kwa niaba yake katika mkataba huu)* Kwa upande mwingine.

**KWA KUWA,** Muuzaji ni mmiliki halali shamba lenye ukubwa wa **ekari** 119.50 **TU** (119.50 TU) tu lenye mipaka asili na amethibitisha mnunuzi kuwa shamba hilo halina deni lolote na wala halijawahi wekewa rehani kwa mtu yeyote, wala taaasisi za kifedha.

**KWA KUWA,** muuzaji kwa hiari yake bila kulazimishwa na mtu ameamua kumuuzia mnunuzi shamba hilo linalojumuisha na mastawio yaliyomo.

**KWA KUWA,** Mnunuzi ana nia ya kununua shamba hilo baada ya kuhakikishiwa na muuzaji shamba hilo halina mgogoro wowote na kwamba atatumia kwa matumizi yake binafsi.

**KWA KUWA,** Mwenyekiti wa kijiji anamfahamu vizuri muuzaji na amethibitisha umiliki wa muuzaji wa shamba hilo.

**KWA KUWA,** wote kwa pamoja wameridhia na kukubali mauziano haya kwa makubaliano yaliyoainishwa hapo chini.

CamScanner

**HIVYO BASI PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO :-**

1. Kwamba, shamba hilo lina ukubwa wa ekari **Mia Moja Kumi na Tisa Na Nusu tu (119.50)** na lina mipaka ya asili ambayo ni;

   Upande wa **mashariki** amepakana na **MOHAMED HUSSEIN BASHE.**

   Upande wa **magharibi** amepakana na. **MOHAME/MWANASENI/MSUTA**

   Upande wa **kaskazini** amepakana na **MOHAMED HUSSEIN BASHE.**

   Upande wa **kusini** amepakana na **MOHAMED HUSSEIN BASHE.**

2. Kwamba, Shamba hilo limeuzwa kwa kiasi cha **shilingi Milioni Mia Moja na Ishirini tu (120,000,000/=)**, ambayo italipwa yote taslimu siku na tarehe ya kusaini makubaliano haya.
3. **Kwamba,** pande zote zimekubaliana kuheshimu na kutii masharti yaliyomo kwenye mkataba huu, na kwamba mkataba huu utawabana pande zote mbili ikiwa ni pamoja na ndugu na jamaa.
4. **Kwamba,** mkataba huu utasomwa na kutafsiriwa kwa mujibu wa sheria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania zinazotumika kwa wakati huu.
5. **Kwamba,** muuzaji anakiri kuwa shamba hili kwa ujumla wala sehemu yake halijawekwa rehani kwa mtu yeyote, taasisi ya kifedha wala chama chochote cha ushirika kama dhamana ya mkopo wowote ule.
6. **Kwamba,** muuzaji atahakikisha wanampa ushirikiano wa karibu mnunuzi na watahakikisha ushirikiano wa karibu mnunuzi na watahakikisha kuwa hakuna tatizo lolote litakalojitokeza juu ya umiliki wa shamba lililotajwa katika utangulinzi wa mkataba huu mara baada ya mauziano haya kukamilika.
7. **Kwamba,** mnunuzi atakuwa huru kulitumia shamba tajwa katika mkataba huu na mastawio yaliyomo kadili yatakavyoona inafaa bila kusumbuliwa na muuzaji, Ndugu zao, familia au mtu yeyote aliye chini ya himaya ya muuzaji mara baada ya mkataba huu kusainiwa.
8. **Kwamba,** ikitokea mgogoro kuhusiana na muuzaji kutosema ukweli juu ya umiliki wa shamba tajwa, basi muuzaji atalazimika kurejesha kiasi chote cha

CS CamScanner

fedha kwa mnunuzi ikiwa ni pamoja na fidia ya usumbufu utakao kuwa umejitokeza.

9. **Kwamba,** mnunuzi atakuwa na haki ya kulitumia shamba tajwa pamoja na mastawio yaliyomo kwa uhuru wake kadili atakavyoona inafaa bila kusumbuliwa muuzaji, mwenza wake, ndugu zake, familia au mtu yeyote aliye chini ya himaya ya muuzaji **Tarehe 31/09/2025.**

**KWA KUTHIBITISHA HAYO YOTE WAHUSIKA WAMETIA SAINI ZAO HAPA CHINI KAMA IFUATAVYO.**

Mkataba umetiwa saini na hawa wafuatao ambao picha zao zimewekwa hapo pembeni na kugongwa mhuri wa viongozi wa maeneo sahihi:

**KWA UPANDE WA MUUZAJI**

Jina: BASU YALUGALA SAHANI **ALAMA YA DOLE GUMBA**



Saini: ……………………………………

Tarehe 31/12/2024

**SHAHIDI WA MUUZAJI**

Jina: EMMANUEL BASU YALUGALA **ALAMA YA DOLE GUMBA**

Saini: EMA

Tarehe 31/12/2024

CamScanner

**SHAHIDI WA MUUZAJI**

JINA.................................................... **ALAMA YA DOLE GUMBAA**

SAINI....................................................

TAREHE..................................................

**KWA UPANDE WA MNUNUZI**

JINA........Bryon ... Mno........ **ALAMA YA DOLE GUMBA**

SAINI....................................................

TAREHE:....31/12/2024..........

**SHAHIDI WA MNUNUZI** **ALAMA YA DOLE GUMBA**

JINA...BENARD E. KABANDI

SAINI....................................................

TAREHE.....31/12/2024.....

**MAKUBALIANO HAYA YAMEFANYIKA MBELE YA MWENYEKITI WA KIJIJI.**

Jina..JUMA HUSSEIN KIGALU

Saini....................................................

Anwani.......610 TABORA.......

Tarehe .........31/12/2024........

SERIKALI YA KIJIJI CHA KINYAMWE
REG/B309004135
WILAYA YA UYUI

**MAKUBALIANO HAYA YAMEFANYIKA MBELE YA MTENDAJI WA KIJIJI.**

Jina...FORTUNATUS HENERICO

Saini....................................................

Anwani.......610 TBR.......

Tarehe .......31/12/2024.

OFISI YA MTENDAJI
KIJIJI CHA KINYAMWE
MAGIRI-UYUI

**MBELE YANGU**

JINA ......................................

SAHIHI ......................................

ANUANI ......................................

WADHIFA **KAMISHNA WA VIAPO**